# SHULE YA SEKONDARI RUHUWIKO
# SHERIA ZA SHULE

| S/No. | AINA YA KOSA | UFAFANUZI WA KOSA | KIWANGO CHA ADHABU |
|---|---|---|---|
| **1.** | **WIZI** | a. Wizi wa mali za shule, wizi wa mali za mwalimu, mwanafunzi mwenzake, mtu yeyote nje au ndani ya shule.<br>b. Mwanafunzi kukamatwa na karatasi yoyote ndani ya chumba cha mtihani mbali na ile ya maswali/kujibia au kukamatwa akiongea au kuoneshana majibu na mwenzake.<br>c. Kumfichia siri mwizi kwa kukataa kumtaja, kwa kuharibu ushahidi au kushirikiana na mwizi katika kutekeleza wizi huo. | Kufukuzwa shule.<br><br>Kufutiwa mtihani unaohusika pamoja na mingine yote atakayokuwa amefanya.<br><br>Kusimamishwa shule mara moja. |
| **2.** | **UASHERATI** | a. Uasherati, kukutwa na barua za mapenzi, kuwa na wapenzi ndani nan je ya shule, kukutwa na kondomu/vidonge vya kuzuia mimba, kupata mimba au kusababisha mimba.<br><br>b. Kutoa mimba au kusaidia kitendo cha kutoa mimba. | Kufukuzwa shule mara moja.<br><br>Kufukuzwa shule mara moja. |
| **3.** | **ULEVI** | a. Ulevi wa aina yoyote kwa mfano pombe na madawa ya kulevya.<br><br>b. Kuonekana katika mabaa au nyumba za wageni (guest house). | Kufukuzwa shule mara moja.<br><br>Mzazi/mlezi kuitwa shuleni na adhabu ya viboko. |
| **4.** | **KOSA LA JINAI** | a. Mwanafunzi yeyote atakayehusika na kosa la jinai<br>b. Mwanafunzi yeyote atakayetiwa hatiani na mahakama. | Kufukuzwa shule mara moja.<br><br>Kufukuzwa shule mara moja. |
| **5.** | **KUPIGANA** | a. Mwanafunzi atakayesababisha ugomvi<br><br>b. Mwanafunzi aliyeanza kumpiga mwenzake au kumkodi mtu mwingine kutimiza lengo hilo. | Kufukuzwa shule mara moja.<br><br>Viboko sita hadharani. |
| **6.** | **KUHARIBU MALI YA UMMA** | a. Kuharibu Mali ya umma, shule, mwalimu au mwanafunzi mwingine, kuinamisha seng'enge na kutoroka/kuingia shuleni. | Kusimamishwa shule siku 21. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **7.** | **KUDHARAU, KUTUKANA NA KASHFA** | a. Kumdharau, kumkashfu na kumtukana mwalimu au kiongozi.<br>b. Kudharau amri halali zilizotolewa.<br>c. Kudharau bendera ya Taifa, wimbo wa Taifa, fedha za nchi na viongozi wa serikali. | Kufukuzwa shule mara moja. |
| **8.** | **KUOA AU KUOLEWA** | a. Yeyote atakayegundulika kuwa ameoa au ameolewa.<br>b. Yeyote atakayegundulika kuwa ana mtoto. | Kufukuzwa shule mara moja. |
| **9.** | **KUGOMA** | a. Yeyote atakayedhibitishwa amegoma adhabu ya kiongozi au mwalimu.<br>b. Kumkimbia mwalimu baada ya kukosa.<br>c. Atakayegoma adhabu au kumtishia mwalimu au kumpiga kiongozi wake. | Atalazimishwa adhabu hiyo mbele ya wenzake. Atakayekubali atatekeleza ataongezewa kusimamishwa shule siku 21.<br>Kosa **b** na **c** atafukuzwa shule. |
| **10.** | **UTORO NA MAHUDHURIO HAFIFU** | Siku moja ya utoro au kukosa shule, utoro uliokithiri zaidi ya siku 21, mwanafunzi wa bweni kulala nje ya shule bila kibali cha uongozi wa shule. | Viboko 4, kumwita mzazi na viboko 6 hadharani, kufukuzwa shule. |
| **11.** | **TAALUMA** | a. Kutohudhuria vipindi, kutoandika, kutofanya najaribio na kazi zozote za kitaaluma.<br><br>b. Kutozungumza kiingereza. Kupata maksi chini ya asilimia 55% kwa kidato cha I hadi IV na asilimia 60% kwa kidato cha V na VI katika majaribio.<br><br>c. Kupata maksi chini ya 55% kwa kidato cha 1 & 3 na chini ya 60% wa kidato cha 5 kama wastani wa mwaka. | Viboko visivyozid 6 kila kosa.<br><br>Viboko visivyozidi 6 kulingana na maksi mtu alizopata.<br><br>Kutafuta shule nyingine au kurudia darasa au kusajiliwa kama mtahiniwa wa kujitegemea kwa kidato cha sita. |
| **12.** | **KUCHELEWA** | a. Yeyote anayechelewa na kufika baada ya 07:15 asubuhi.<br>b. Yeyote anayechelewa kuingia darasani, kwenda mstarini, kuripoti anapoitwa au kufika nyumbani.<br>c. Atakayechelewa kwenye chumba cha mtihani zaidi ya nusu saa. | Onyo kali na viboko 4.<br><br>Hatafanya mtihani unaohusika. |
| **13.** | **MIPAKA YA SHULE** | Kila mwanafunzi anatakiwa kuwepo pale anapostahili wakati wowote kufuatana na taratibu za shule.<br>Ruhusa itatolewa na mwalimu pale mwanafunzi anapostahili kwenda sehemu nyingine.<br>Sehemu zifuatazo ni nje na mipaka ya shule: - chumba cha walimu, ofisi ya shule, maabara ya hospitali, ofisi za kikosi na nyumba za kuishi | Atakayeonekana nje ya mipaka ya shule viboko visivyozidi 6 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | kikosini.<br>Ni marufuku kusimama bila sababu nje ya mlango wa kuingia shule. | |
| **14.** | **SARE YA SHULE** | a. Kuvaa sare isiyo ya shule<br>b. Mshono usio wa heshima<br>c. Kaptura au sketi fupi au ndefu mno<br>d. Kutovaa necktie, strips au skai, nembo ya shule.<br>e. Sare chafu au iliyochanika<br>f. Kuvaa sketi au kaptura zaidi ya moja.<br>g. Nywele ndefu, kunyoa kihuni, kuweka dawa nywele.<br>h. Kufuga ndevu na kucha.<br>i. Kuvaa mapambo. | Viboko visivyozidi 6 |
| **15.** | **HESHIMA, UTII NA UAMINIFU** | a. Mwanafunzi asiyesalimu walimu na yeyote anayemzidi umri.<br>b. Asiyetii amri aliyopewa na mwalimu, kiongozi au mkubwa yeyote.<br>c. Mwanafunzi mwongo, mmbea au asiyemwaminifu au mchonganishi. | Onyo kali na adhabu ya viboko visivyozidi 6. |
| **16.** | **FUJO NA KELELE** | Fujo na kelele darasani, mstarini, bwenini, mikutanoni au eneo lolote la shule. | Adhabu ya mazoezi ya mwili na viboko. |
| **17.** | **AFYA** | a. Kula vyakula ovyo ovyo njiani au sehemu zisizoruhusiwa na shule, kutafuna tafuna ovyo darasani au ofisi ya walimu au mstarini, kutupa au kutookota uchafu unaomzunguka, kutovaa nadhifu.<br>b. Kutupa tupa ovyo uchafu na kutosafisha sehemu aliyopangiwa. | Onyo na viboko visivyozidi 4. |

**NB:-**

1. Adhabu zilizotajwa hapo juu hazihusishi adhabu za mazoezi ya viungo, kulima, kusafisha maeneo n.k. Adhabu zote zitatolewa kulingana na uzoefu wa mtu kufanya makosa. Kukiri kwake na kuomba msamaha au kukataa na usumbufu kwa mwalimu.

2. Makosa mengine yasiyotajwa hapo juu yatashughurikiwa na walimu kulingana na uzito wa kosa husika.